# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

## MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA

# RIPOTI YA ZOEZI LA USAJILI NA UTAMBUZI WA WANANCHI WILAYA YA SONGEA

**April 2017 – June 2018**

OFISI YA USAJILI NA UTAMBUZI

WILAYA YA SONGEA

S L P 734

SONGEA-RUVUMA

## YALIYOMO


**1. UTANGULIZI ..........2**

**2. UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA USAJILI..........2**

2.1. USHIRIKI WA VIONGOZI WA WILAYA..........3

2.2. USHIRIKI WA VIONGOZI WA KATA NA MITAA/VIJIJI..........3

2.3. USHIRIKI WA IDARA YA UHAMIAJI..........3

2.4. ULINZI NA USALAMA..........4

2.5. HALI YA USAFIRI..........4

2.6. UHALISIA WA TAKWIMU YA WANANCHI KATIKA MITAA NA VIJIJI..........4

**3. MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA ZOEZI KWA NGAZI YA KATA NA MITAA/VIJIJI..........5**

3.1. TAKWIMU ZA USAJILI HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA..........5

3.2. TAKWIMU ZA USAJILI HALMASHAURI YA SONGEA VIJIJINI..........8

3.3. TAKWIMU ZA USAJILI HALMASHAURI YA MADABA..........11

**4. CHANGAMOTO..........13**

**5. MAFANIKIO..........15**

**6. SHUKRANI..........15**

6.1. OFISI YA MKUU WA WILAYA..........15

6.2. OFISI ZA WAKURUGENZI WA HALMASHAURI..........16

6.3. OFISI YA UHAMIAJI..........17

6.4. OFISI YA NIDA MAKAO MAKUU..........17

**7. HITIMISHO..........17**

## 1. UTANGULIZI.

Ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Wilaya ya Songea ilianza zoezi la Utambuzi na Usajili wa Wananchi mnamo mwezi Aprili 2017 baada ya kukamilika kwa zoezi la Usajili na Utambuzi wa Watumishi wa Umma lililoanza October 03,2016.Ofisi ya Wilaya iliendelea na, zoezi la kuhudumia wananchi waishio kata jirani na Ofisi huku tukiwa tunasubiri kupokea vifaa vya usajili (BVR kit) pamoja na rasilimali fedha za kuwezesha zoezi la Usajili wa Umma (Mass Registration) ambalo huduma ya usajili hutolewa katika ngazi za mitaa/vijiji wanapoishi waombaji wa Vitambulisho vya Taifa.

## 2. UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA USAJILI.

Baada ya kupokea vifaa vya usajili mnamo mwezi Disemba 2017, na kumalizika kwa uzinduzi uliofanywa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani Ndugu Mwigulu Nchemba mnamo tarehe 29/12/2017, Ofisi ya NIDA Wilaya ya Songea ilianza rasmi zoezi la Utambuzi na Usajili wa Wananchi tarehe 2/1/2018.

Wilaya ya Songea ina Halmashauri tatu ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea ambayo inakadiriwa kuwa na Wananchi wenye sifa ya kusajiliwa wapatao laki moja, hamsini na mbili elfu, mia tatu sabini na tano **(152,375)**.Ikifuatiwa na Halmashauri ya Songea Vijijini yenye Wananchi wenye sifa ya kusajiliwa wapatao Elfu sabini na nne, mia moja na arobaini na saba **(74,147)**, na Halmashauri ya Madaba yenye Wananchi wenye sifa ya kusajiliwa wapatao Elfu ishirini na saba, mia tisa na thelathini na moja **(27,931)**.

Kwa ujumla ya Halmashauri zote tatu,Wilaya ya Songea inakadiriwa kuwa na jumla ya Wananchi laki mbili,hamsini na nne elfu,mia nne na hamsini na tatu **(254,453)** wenye sifa ya kusajiliwa ambao ni wenye umri wa miaka kumi na nane na kuendelea.

Tulianza zoezi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa utaratibu wa awamu (Phases) ambapo kwa Manispaa tumefanikiwa kukamilisha zoezi kwa kutumia awamu nne kwa kusajili wananchi Elfu tisini na tano na Hamsini na tano **(95,055)** kati ya Wananchi Laki moja Hamsini na mbili elfu,mia tatu na Sabini na

tano **(152,375)** sawa na asilimia **62.38.**Kwa Halmashauri ya Songea Vijijini tumefanikiwa kukamilisha zoezi kwa awamu mbili kwa kusajili Wananchi Elfu Hamsini na sita, Mia saba na Sitini na sita **(56,766)** kati ya Wananchi Elfu Sabini na nne,Mia moja na robaini na saba **(74,147)** sawa na asilimia **76.56** na Halmashauri ya Madaba tumefanikiwa kwa kutumia awamu mbili na kusajili wananchi Elfu Ishirini na tatu na mbili'**(23,002)** kati ya Wananchi Elfu Ishirini na saba,Mia tisa na thelathini na moja **(27,931)** sawa na asilimia **82.5**

## 2.1. USHIRIKI WA VIONGOZI WA WILAYA.

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Wilaya ya Songea imepata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa Viongozi wa Wilaya akiwemo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Songea,Katibu Tawala wa Wilaya,Wakurugenzi wa Halmashauri zote tatu pamoja na Ofisi ya Afisa Usalama wa Wilaya,kwa pamoja wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha zoezi linafanyika kwa ufanisi na ushirikiano mkubwa sana.

## 2.2. USHIRIKI WA VIONGOZI WA KATA NA MITAA/VIJIJI.

Ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Songea imepata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa viongozi wa Kata, Mitaa/ Vjijiji, Wenyeviti wa Mitaa/Vijiji bila kusahau Waheshimiwa Madiwani.Kwa pamoja wameweza kushiriki kikamilifu katika swala nzima la uhamasishaji, kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa Vitambulisho vya Taifa, na pia wamepambana kuhakikisha Maafisa katika zoezi la Usajili wanapata Malazi, Chakula na Ulinzi wa vifaa kwa siku zote za zoezi.

## 2.3. USHIRIKI WA IDARA YA UHAMIAJI

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Wilaya ya Songea imeshirikiana na Maafisa Uhamiaji kikamilifu na kuweza kufikia malengo ya kuwatambua na kuwahoji wananchi wote walioshiriki katika zoezi la Usajili na Utambuzi wa watu.Katika utekelezaji wa zoezi Maafisa Uhamiaji waliweza kufika kila kijiji na kuweza kufanya mahojiano ana kwa ana na kila mwananchi.Aidha katika mahojiano hayo ya kudhibitisha uraia wa mwombaji wa Kitambulisho,mpaka sasa Wananchi zaidi

ya Elfu nne **(4000)** wanahitajika kufanyiwa mahojiano ya kina kwani Maafisa Uhamiaji hawakuweza kujiridhisha na taarifa zao za kiuraia.

## 2.4. ULINZI NA USALAMA

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Songea imefanikiwa kutekeleza zoezi la Usajili wa Wananchi wa Halmashauri zote tatu kwa hali ya amani na utulivu.Kamati ya Ulinzi na Usalama imehakikisha zoezi linafanyika kwa usalama mkubwa kama ilivyokuwa imeahidiwa na imetekelezwa hivyo.Hapakuwa na hali yoyote ya vitisho vya uvunjifu wa amani katika kipindi chote cha zoezi, usalama wa Maafisa na Vifaa ulikuwa wa kutosha.

## 2.5. HALI YA USAFIRI.

Ofisi ya NIDA Wilaya ya Songea imeweza kupata ushirikiano wa kutosha kutoka Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri katika swala nzima la upatikanaji wa magari kwa ajili ya kusafirisha Maafisa na Vifaa kwenda kwenye maeneo mbalimbali ya kazi.Licha ya kwamba ofisi za Halmashauri zilihitaji usafiri kwa shughuli zake za kiofisi,ila Wakurugenzi wa kila Halmashari walifanikisha kututengea gari ambalo tulilitumia muda wote wa kazi,na pindi tulipohitaji magari zaidi ya moja waliweza kutupatia hususani wakati wa kuhamisha vifaa na Maafisa kutoka sehemu moja kwenda sehemu zingine.

## 2.6. UHALISIA WA TAKWIMU YA WANANCHI KATIKA MITAA NA VIJIJI.

Kabla ya kuanza kwa zoezi la usajili,tuliweza kuwasiliana na Maafisa Takwimu wa Halmashauri zote tatu na kuweza kupatiwa takwimu za wananchi wenye sifa ya kusajiliwa ambao wana umri wa miaka kumi na nane na kuendelea.Kupitia takwimu hizo ndipo tuliweza kuaandaa mpango kazi kwa njia ya awamu.Changamoto ilikuja hususani kwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea ambapo takwimu tulizopewa za baadhi ya mitaa hazikuwa na uhalisia na Idadi ya wananchi kwenye mtaa husika.Takwimu zilikuwa zipo juu ukilinganisha na idadi ya wananchi wenye sifa ya kusajiliwa kwenye baadhi ya mitaa,na tuliweza kudhibitishiwa na baadhi ya watendaji wa mitaa ya kuwa hizo takwimu ni za

ujumla wa wananchi wote na si pekee wenye sifa ya miaka 18 na kuendelea.Kwa upande wa zoezi ilitupa changamoto sana katika kupanga mgawanyo wa mashine na Maafisa waliohitajika.

## 3. MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA ZOEZI KWA NGAZI YA KATA NA MITAA/VIJIJI

| 3.1 TAKWIMU ZA USAJILI WA WANANCHI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KATA** | **MTAA/KIJIJI** | **LENGO WATU** | **WALIOANDIKISHWA** | **ASILIMIA** |
| 1.BOMBAMBILI | Merikebu | 4771 | 3160 | 66.23 |
| | Miembeni | 3803 | 1835 | 48.25 |
| | Mtakuja | 3841 | 1815 | 47.25 |
| | Muungano | 3904 | 956 | 24.49 |
| | Sokoine | 3290 | 1249 | 37.96 |
| | **JUMLA(Kata)** | **19609** | **9015** | **45.97** |
| | | | | |
| 2.LILAMBO | Likuyufusi | 1324 | 833 | 62.92 |
| | Lilambo 'B' | 1288 | 696 | 54.04 |
| | Lilambo 'A' | 1358 | 900 | 66.27 |
| | Luwawasi | 667 | 270 | 40.48 |
| | Mang'ua | 1196 | 508 | 42.47 |
| | Mwanamonga | 858 | 623 | 72.61 |
| | Myegeya | 848 | 467 | 55.07 |
| | Sinai | 834 | 583 | 69.90 |
| | **JUMLA(Kata)** | **8373** | **4880** | **58.28** |
| 3.LIZABONI | | | | |
| | Kibulang'oma | 2097 | 1201 | 57.27 |
| | Londoni | 1000 | 1161 | 116.10 |
| | Madizini | 2746 | 1226 | 44.65 |
| | Mloweka | 2145 | 1079 | 50.30 |
| | Polisi | 3053 | 768 | 25.16 |
| | Sokoni | 2373 | 1647 | 69.41 |
| | **JUMLA(Kata)** | **13414** | **7082** | **52.80** |
| 4.MAJENGO | | | | |
| | Kotazi | 1862 | 950 | 51.02 |
| | Matuli | 1142 | 724 | 63.40 |
| | M/Mkuu Moyo | 2168 | 1177 | 54.29 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5172** | **2851** | **55.12** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **5.MATARAWE** | Asia Kovu | 2118 | 908 | 42.87 |
| | Msafiri | 1322 | 714 | 54.01 |
| | Sabasaba | 1417 | 834 | 58.86 |
| | **JUMLA(Kata)** | **4857** | **2456** | **50.57** |
| **6.MATEKA** | | | | |
| | Mateka 'A' | 1342 | 862 | 64.23 |
| | Mateka 'B' | 1201 | 1060 | 88.26 |
| | Mateka 'C' | 1882 | 871 | 46.28 |
| | **JUMLA(Kata)** | **4425** | **2793** | **63.12** |
| **7.MATOGORO** | | | | |
| | Chemchem | 915 | 520 | 56.83 |
| | Mahiro | 681 | 314 | 46.11 |
| | Mkwawa | 881 | 486 | 55.16 |
| | Matogoro Kati | 1107 | 540 | 48.78 |
| | **JUMLA(Kata)** | **3584** | **1860** | **51.90** |
| **8.MFARANYAKI** | | | | |
| | Bilauri | 1380 | 590 | 42.75 |
| | Matomondo | 1523 | 709 | 46.55 |
| | Mbalika | 1835 | 658 | 35.86 |
| | Mfaranyaki | 1633 | 902 | 55.24 |
| | **JUMLA(Kata)** | **6371** | **2859** | **44.88** |
| **9.MISUFINI** | | | | |
| | Mabatini | 1290 | 565 | 43.80 |
| | Majimaji | 774 | 345 | 44.57 |
| | Msikitini | 1151 | 410 | 35.62 |
| | **JUMLA(Kata)** | **3215** | **1320** | **41.06** |
| **10.MJIMWEMA** | | | | |
| | Misufini | 804 | 959 | 119.28 |
| | Mjimwema 'A' | 1972 | 1452 | 73.63 |
| | Mjimwema 'B' | 1968 | 1509 | 76.68 |
| | Pachanne 'A' | 3014 | 1230 | 40.81 |
| | Pachanne 'B' | 663 | 996 | 150.23 |
| | **JUMLA(Kata)** | **8421** | **6146** | **72.98** |
| **11.MJINI** | | | | |
| | C.C.M | 1279 | 718 | 56.14 |
| | Mahenge | 2038 | 991 | 48.63 |
| | Mashujaa | 2273 | 827 | 36.38 |
| | Mpambalyoto | 1009 | 2334 | 231.32 |
| | **JUMLA(Kata)** | **6599** | **4870** | **73.80** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12.MLETELE | Liwumbu | 422 | 209 | 49.53 |
| | Makemba | 262 | 102 | 38.93 |
| | Mdundiko | 1153 | 655 | 56.81 |
| | Mjimwema | 389 | 212 | 54.50 |
| | Mletele | 1024 | 808 | 78.91 |
| | Nonganonga | 476 | 186 | 39.08 |
| | **JUMLA(Kata)** | **3726** | **2172** | **58.29** |
| 13.MSAMALA | | | | |
| | Making'inda | 3519 | 1758 | 49.96 |
| | Miembeni | 6098 | 1760 | 28.86 |
| | Mkuzo | 3719 | 2264 | 60.88 |
| | Mtaungana | 2385 | 1641 | 68.81 |
| | Oysterbay | 3406 | 2171 | 63.74 |
| | **JUMLA(Kata)** | **19127** | **9594** | **50.16** |
| 14.MSHANGANO | | | | |
| | Mitendewawa | 553 | 364 | 65.82 |
| | Mshangano | 2970 | 2622 | 88.28 |
| | Chandarua | 783 | 455 | 58.11 |
| | Muhombezi | 441 | 266 | 60.32 |
| | Namanyigu | 988 | 1233 | 124.80 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5735** | **4940** | **86.14** |
| 15.M/MSHINDO | | | | |
| | M/Mshindo | 1207 | 821 | 68.02 |
| | Ruhila Kati | 611 | 395 | 64.65 |
| | **JUMLA(Kata)** | **1818** | **1216** | **66.89** |
| 16.NDILIMALITEMBO | | | | |
| | Makambi | 3648 | 1745 | 47.83 |
| | Matogoro Shuleni | 1388 | 970 | 69.88 |
| | Ndilimalitembo | 1125 | 764 | 67.91 |
| | **JUMLA(Kata)** | **6161** | **3479** | **56.47** |
| 17.RUHUWIKO | | | | |
| | Namanditi | 912 | 721 | 79.06 |
| | Ruhuwiko 'C' | 1306 | 1198 | 91.73 |
| | Ru/ Kanisani | 968 | 1019 | 105.27 |
| | Ru/ Shuleni | 1970 | 1797 | 91.22 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5156** | **4735** | **91.83** |
| 18.RUVUMA | | | | |
| | Mbulani 'A' | 1299 | 1612 | 124.10 |
| | Mbulani 'B' | 2097 | 1367 | 65.19 |
| | Ruvuma Chini | 4532 | 3143 | 69.35 |
| | Ruvuma Juu | 1536 | 1463 | 95.25 |
| | **JUMLA(Kata)** | **9464** | **7585** | **80.15** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19.SEEDFARM | Kuchile | 1168 | 732 | 62.67 |
| | Ruhila | 1558 | 531 | 34.08 |
| | Ruhila Seko | 2184 | 1324 | 60.62 |
| | Unangwa | 801 | 446 | 55.68 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5711** | **3033** | **53.11** |
| 20.SUBIRA | | | | |
| | Kihekwa | 881 | 470 | 53.35 |
| | Kisiwani 'C' | 745 | 394 | 52.89 |
| | Lami | 669 | 399 | 59.64 |
| | Mahinya | 920 | 575 | 62.50 |
| | Muungano | 607 | 352 | 57.99 |
| | Nangwahi | 311 | 141 | 45.34 |
| | Ngandula | 523 | 328 | 62.72 |
| | Subira Kati | 700 | 474 | 67.71 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5356** | **3133** | **58.50** |
| 21.TANGA | | | | |
| | Masigira | 942 | 415 | 44.06 |
| | Mitawa | 850 | 467 | 54.94 |
| | Mlete | 1295 | 503 | 38.84 |
| | Pambazuko | 689 | 743 | 107.84 |
| | Sanangula | 727 | 729 | 100.28 |
| | Tanga | 1578 | 1200 | 76.05 |
| | **JUMLA(Kata)** | **6081** | **4057** | **66.72** |
| | **WATUMISHI WA UMMA** | | **4979**<br>**90076** | |
| | **JUMLA KUU** | **152375** | **95055** | **62.38** |

## 3.2 TAKWIMU ZA USAJILI WA WANANCHI WA HALMASHAURI YA SONGEA VIJIJINI

| KATA | MTAA/KIJIJI | LENGO WATU | WALIOANDIKISHWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1.LILAHI | Magwamila | 566 | 474 | 83.75 |
| | Makwaya | 761 | 873 | 114.72 |
| | Muhukuru Lilahi | 2339 | 1451 | 62.04 |
| | **JUMLA(Kata)** | **3666** | **2798** | **76.32** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2.MUHUKURU | Maniamba | 1245 | 903 | 72.53 |
| | Mipeta | 990 | 855 | 86.36 |
| | Muhukuru Barabarani | 2033 | 1914 | 94.15 |
| | Muhukuru Nakawale | 1814 | 1552 | 85.56 |
| | **JUMLA(Kata)** | **6082** | **5224** | **85.89** |
| 3.NDONGOSI | | | | |
| | Namatuhi | 1522 | 1243 | 81.67 |
| | Nambendo | 733 | 767 | 104.64 |
| | Ndongosi | 1504 | 880 | 58.51 |
| | **JUMLA(Kata)** | **3759** | **2890** | **76.88** |
| 4.MPITIMBI | | | | |
| | Lipaya | 1848 | 1496 | 80.95 |
| | Mpitimbi 'A' | 2400 | 1335 | 55.63 |
| | Mpitimbi 'B' | 1432 | 1071 | 74.79 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5680** | **3902** | **68.70** |
| 5.LITAPWASI | | | | |
| | Litapwasi | 1007 | 527 | 52.33 |
| | Lyangweni | 1022 | 823 | 80.53 |
| | Uyahudini | 855 | 583 | 68.19 |
| | **JUMLA(Kata)** | **2884** | **1933** | **67.02** |
| 6.MATIMIRA | | | | |
| | Kikunja | 759 | 409 | 53.89 |
| | Liula | 2080 | 1120 | 53.85 |
| | Matimira 'A' | 1178 | 772 | 65.53 |
| | Matimira 'B' | 908 | 483 | 53.19 |
| | Mpangula | 493 | 346 | 70.18 |
| | Mpingi | 1145 | 761 | 66.46 |
| | **JUMLA(Kata)** | **6563** | **3891** | **59.29** |
| 7.MAGAGURA | | | | |
| | Lusonga | 1472 | 1242 | 84.38 |
| | Magagura | 2128 | 1787 | 83.98 |
| | Masangu | 1344 | 761 | 56.62 |
| | **JUMLA(Kata)** | **4944** | **3790** | **76.66** |
| 8.KIZUKA | | | | |
| | Kizuka | 1556 | 1798 | 115.55 |
| | Mbiro | 1146 | 691 | 60.30 |
| | Ngahokora | 2039 | 1351 | 66.26 |
| | **JUMLA(Kata)** | **4741** | **3840** | **81.00** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.MBINGA MHARULE** | Lipokela | 1163 | 1324 | 113.84 |
| | Matomondo | 900 | 693 | 77.00 |
| | Mbinga mharule | 1547 | 930 | 60.12 |
| | Nakahegwa | 1449 | 1068 | 73.71 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5059** | **4015** | **79.36** |
| **10.PERAMIHO** | | | | |
| | Lundusi | 854 | 779 | 91.22 |
| | Nguvumoja | 857 | 861 | 100.47 |
| | Peramiho 'A' | 2805 | 1816 | 64.74 |
| | Peramiho 'B' | 3166 | 1799 | 56.82 |
| | **JUMLA(Kata)** | **7682** | **5255** | **68.41** |
| **11.LIGANGA** | | | | |
| | Liganga | 1054 | 1126 | 106.83 |
| | Mbolongo | 486 | 605 | 124.49 |
| | Serikano | 897 | 888 | 99.00 |
| | **JUMLA(Kata)** | **2437** | **2619** | **107.47** |
| **12.LITISHA** | | | | |
| | Litisha | 1493 | 1093 | 73.21 |
| | Magima | 1237 | 823 | 66.53 |
| | Morogoro | 1728 | 1160 | 67.13 |
| | Nakahuga | 1509 | 1148 | 76.08 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5967** | **4224** | **70.79** |
| **13.MAPOSENI** | | | | |
| | Maposeni | 1334 | 917 | 68.74 |
| | Mdunduwalo | 1056 | 873 | 82.67 |
| | **JUMLA(Kata)** | **2390** | **1790** | **74.90** |
| **14.KILAGANO** | | | | |
| | Kilagano | 1598 | 1077 | 67.40 |
| | Lugagara | 1530 | 1171 | 76.54 |
| | Mgazini | 2272 | 1540 | 67.78 |
| | Mhepai | 811 | 1080 | 133.17 |
| | Muungano Zomba | 1040 | 708 | 68.08 |
| | **JUMLA(Kata)** | **7251** | **5576** | **76.90** |
| **15.MPANDANGINDO** | | | | |
| | Kituro | 618 | 451 | 72.98 |
| | Liweta | 654 | 459 | 70.18 |
| | Mpandangindo | 1480 | 1167 | 78.85 |
| | **JUMLA(Kata)** | **2752** | **2077** | **75.47** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 16.PARANGU | Chiwurungi | 647 | 192 | 29.68 |
| | Litowa | 531 | 658 | 123.92 |
| | Parangu | 1112 | 748 | 67.27 |
| | **JUMLA(Kata)** | **2290** | **1598** | **69.78** |
| | **WATUMISHI WA UMMA** | | **1344**<br>**55422** | |
| | **JUMLA KUU** | **74147** | **56766** | **76.56** |

| **3.3 TAKWIMU ZA USAJILI WA WANANCHI WA HALMASHAURI YA MADABA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KATA** | **MTAA/KIJIJI** | **LENGO WATU** | **WALIOANDIKISHWA** | **ASILIMIA** |
| 1.WINO | | | | |
| | Igawisenga | 670 | 554 | 82.69 |
| | Lilondo | 2756 | 1670 | 60.60 |
| | Wino | 1073 | 1061 | 98.88 |
| | **JUMLA(Kata)** | **4499** | **3285** | **73.02** |
| 2.MATUMBI | | | | |
| | Ifinga | 1085 | 673 | 62.03 |
| | **JUMLA(Kata)** | **1085** | **673** | **62.03** |
| 3.MATETEREKA | | | | |
| | Matetereka | 738 | 401 | 54.34 |
| | Maweso | 1106 | 757 | 68.44 |
| | Mwande | 804 | 621 | 77.24 |
| | **JUMLA(Kata)** | **2648** | **1779** | **67.18** |
| 4.GUMBIRO | | | | |
| | Gumbiro | 1112 | 2728 | 80.64 |
| | Mbangamawe | 476 | | |
| | Ngadinda | 1795 | | |
| | **JUMLA(Kata)** | **3383** | **2728** | **80.64** |
| 5.MAHANJE | | | | |
| | Madaba | 1173 | 1036 | 88.32 |
| | Mahanje | 1099 | 1105 | 100.55 |
| | **JUMLA(Kata)** | **2272** | **2141** | **94.23** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6.MTYANGIMBOLE | Likarangiro | 1341 | 1006 | 75.02 |
| | Luhimba | 1796 | 1425 | 79.34 |
| | Mtyangimbole | 2427 | 1914 | 78.86 |
| | **JUMLA(Kata)** | **5564** | **4345** | **78.09** |
| 7.LITUTA | | | | |
| | Kipingo | 896 | 713 | 79.58 |
| | Lituta | 2277 | 2160 | 94.86 |
| | Mtepa | 1461 | 1406 | 96.24 |
| | **JUMLA(Kata)** | **4634** | **4279** | **92.34** |
| 8.MKONGOTEMA | | | | |
| | Lutukira | 1486 | 1083 | 72.88 |
| | Magingo | 1034 | 826 | 79.88 |
| | Mkongotema | 1326 | 1317 | 99.32 |
| | **JUMLA(Kata)** | **3846** | **3226** | **83.88** |
| | **WATUMISHI WA UMMA** | | **546**<br>**22456** | |
| | **JUMLA KUU** | **27931** | **23002** | **82.35** |

## 4. CHANGAMOTO

Wakati wa utekelezaji wa usajili wa wananchi kwa awamu zote Wilayani Songea kulijitokeza changamoto kadhaa kama ifuatavyo:

### 4.1. Msimu wa mvua na shughuli za kilimo.

Zoezi la usajili liliadhiriwa sana na kutojitokeza kwa wananchi wa wingi kutokana na mvua nyingi kunyesha na wananchi wengi kuhamia mashambani kuendelea na shughuli za kilimo.Kwa hali ya hewa ya Songea, kuanzia mwezi Disemba hadi Mei ni msimu wa mvua, hivyo zoezi liliadhirika na hiyo hali kwa kuchukua muda mrefu kuwapata walengwa na kupelekea kurudia zoezi maeneo ambayo wakazi wengi walikuwa mashambani mwanzoni mwa zoezi.

### 4.2. Miundombinu korofu kwa baadhi ya maeneo.

Ubovu wa barabara kwa baadhi ya maeneo ulipelekea zoezi kufanyika kwa ugumu kidogo kutokana na kushindwa kuwafikia wananchi kwa muda tulioupanga.Wakati mwingine ilitulazimu kutumia usafiri wa pikipiki kusafirisha Mashine (BVR) pamoja na Operators.

### 4.3. Ukosefu wa Nishati ya Umeme

Maeneo mengi ya Halmashauri ya Songea vijijini na Madaba hayana nishati ya umeme, hivyo wananchi wengi walisumbuka kufata huduma ya photocopy maeneo mengine ambayo asilimia kubwa yalikuwani ya mbali, hivyo kupelekea zoezi kuchelewa kuisha kwa muda uliopangwa kwenye kijiji husika kwa kusubiria nakala za viambata vya wananchi.

### 4.4. Wananchi kutoshiriki zoezi la Usajili wa awali.

Ofisi ya NIDA Songea iliweza kusambaza vifaa vya usajili kwenda ngazi ya Kata,mitaa na vijiji kwa kusaidiwa usafiri kutoka kwenye Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri  ili wananchi waweze kujaziwa fomu halafu ndipo zoezi la kupiga picha na kuchukuliwa alama za vidole lingefuata ili kuokoa muda.Ila kwa  baadhi

ya maeneo wananchi wengi hawakujitokeza kusajiliwa kwenye zoezi la ujazaji fomu,na wengi wao waliweza kujitokeza wakati wa kuanza kwa zoezi la kupiga picha na kuchukuliwa alama za vidole hivyo kupelekea zoezi kuchukua muda mrefu kwani Watendaji wa Mitaa na Vijiji walilazimika kuwajazia fomu wananchi wapya na pia kuwagawia fomu wale waliojiandikisha awali ili wote waweze kupigwa picha na kuchukuliwa alama za vidole.

### 4.5. Kukosekana kwa Postcode kwa baadhi ya vijiji.

Tulipata changamoto ya kutokuwepo kwa postcode ya Vijiji viwili kwenye kata ya Gumbiro katika Halmashauri ya Madaba ambavyo ni kijiji cha Ngadinda na Mbangamawe.Lilikuwa ni tatizo la kimfumo na hivyo ilitulazimu kutumia kijiji kimoja tu cha Gumbiro wakati wa zoezi katika kata hiyo.Ilitulazimu kufanya hivyo kwa sababu tulishapanga ratiba na wananchi walishakusanyika kwa ajili ya kupatiwa huduma ,hivyo kuhairishwa kwa zoezi kungeleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi.Baada ya kuwasilisha changamoto hiyo ofisini,tatizo liliweza kutatuliwa.

### 4.6. Changamoto ya Uhamasishaji kwa awamu za mwanzo wa zoezi.

Mwanzoni mwa zoezi tulipata changamoto kutoka kwa wenyeviti na watendaji wa mitaa kwa kushindwa kuhamasisha wananchi waweze kujitokeza kwa wingi wakati wa zoezi na kupeleka kupata takwimu duni kwa awamu ya kwanza.Tuliweza kuripoti changamoto hiyo kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea na pia kwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Songea ambaye aliweza kuitisha kikao kilichohudhuriwa na Waheshimiwa Madiwani,Maafisa Tarafa,Watendaji wa Kata,Mitaa na Wenyeviti kutoka kwenye kata za awamu ya kwanza ambazo ni Ndilimalitembo,Seedfarm,Matogoro na Mletele na kuweza kuwasisitizia kufanya uhamasishaji kwa wananchi.Baada ya kikao hicho,ofisi ya NIDA iliweza kupanga ratiba ya marudio ya zoezi kwenye kata hizo nne na kuweza kufanikiwa baada ya Waheshimiwa Madiwani,Wenyeviti na Watendaji kufanya uhamasishaji wa kutosha.

### 4.7. Uhalisia wa Takwimu ya Watu ngazi ya Mitaa/Vijiji.

Kabla ya kuanza kwa zoezi,Ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa wilaya ya Songea iliweza kuwasiliana na Maafisa Takwimu kwenye kila Halmashauri na kutupatia katwimu za wananchi wenye umri wa miaka kumi na nane na kuendelea ambao ndio wenye sifa ya kusajiliwa.Kwa kupitia takwimu hizo ndipo tuliweza kuandaa mpango kazi kwa kufuata utaratibu wa awamu (Phases).Changamoto kubwa tuliyoipata ni uhalisia wa takwimu ya wananchi ngazi ya mitaa na vijiji hususani katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwani takwimu tulizopewa ni kubwa kuliko idadi halisi ya wananchi wenye sifa ya kusajiliwa kwenye baadhi ya mitaa,na tulidhibitishiwa na watendaji katika mitaa husika kuwa ni takwimu zilizowakilisha watu wote kwenye mtaa na si pekee wenye miaka kumi na nane na kuendelea.Hali hiyo ilitupa changamoto kubwa katika ugawaji wa mashine na idadi ya Maafisa waliohitajika.

## 5. MAFANIKIO KWA UJUMLA.

Licha ya kuwepo kwa changamoto wakati wa zoezi ila tuliweza kufanikiwa kwa kiwango cha kuridhisha kwa kutanguliza uzalendo na kufanya kazi katika mazingira ya mvua na changamoto zingine mbalimbali.Ofisi ya NIDA Wilaya imefanikiwa kusajili wananchi laki moja sabini na nne elfu, mia nane na ishirini na tatu **(174,823)** kati ya wananchi Laki mbili Hamsini na nne Elfu, Mia nne na hamsini na tatu **(254,453)** sawa na asilimia **68.81.**

## 6. SHUKRANI

### 6.1. OFISI YA MKUU WA WILAYA.

Ofisi ya NIDA Wilaya ya Songea inapenda kuishukuru Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Songea kwa kusimamia na kuhakikisha zoezi la Usajili wa Wananchi wa Wilaya ya Songea linaendeshwa kwa hali ya amani na utulivu

mkubwa na kila mwananchi mwenye sifa aliyejitokeza kusajiliwa, amehudumiwa kikamilifu.

Aidha Ofisi ya NIDA Songea inatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Songea pamoja na Katibu Tawala wa Wilaya kwa kuhakikisha usajili unafanyika vizuri na kuwahamasisha Kamati ya Ulinzi na Usalama inashiriki kikamilifu katika utoaji wa Elimu na Uhamasishaji, kuwahamasisha Waheshimiwa Madiwani, Watendaji, Wenyeviti na Wananchi kuwakarimu Maafisa wa Usajili pindi wanapokuwa katika Mitaa na Vijiji vyao wakati wa zoezi.

## 6.2. OFISI YA MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA, HALMASHAURI YA SONGEA VIJIJINI NA HALMASHAURI YA MADABA.

Ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Wilaya ya Songea inapenda kuwashukuru Wakurugenzi wa Halmashauri zote tatu za Wilaya ya Songea kwa kuhakikisha watendaji wote wa Kata,Mitaa na Vijiji wanakuwepo na kushiriki wakati wote wa zoezi na wanasimamia ulinzi wa Vifaa na Maafisa katika maeneo yao.Aidha Wakurugenzi wamehakikisha upatikaji wa rasilimali zote zilizohitajika wakati wa zoezi mfano magari n.k na upatikanaji wa Operators ambao wengi wao walikuwa ni Watumishi wa Umma kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea ambao wamesaidia sana kuhakikisha zoezi linafanikiwa kwa kutumia vizuri taaluma zao na wameweza kuvumilia changamoto zote na kufanya kazi kwa uzalendo zaidi.

Tunatoa pongezi pia kwa Waratibu wa NIDA ngazi ya Halmashauri (Focal Persons) ambao walichaguliwa na Wakurugenzi wa Halmashauri ambao kiukweli wametusaidia sana katika kufanikisha zoezi la usajili kwani wameweza kutuandalia mazingira ya kazi kupitia kwa watendaji wa vijiji na kutusaidia kutatua changamoto ndogo ndogo zilizojitokeza wakati wa usajili vijiji na mjini.

Ofisi pia inapenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Madiwani, Watendaji, Wajumbe,Mabalozi na Wenyeviti wote wa Mitaa na Vijiji katika Halmashauri zote tatu za Songea kwa kuweza kulipokea zoezi katika Kata na vijiji vyao na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa kuhamasisha wananchi kuweza kujitokeza kusajiliwa ili dhumuni la Serikali liweze kukamilika.